



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma Ndugu Godwin Kunambi anapenda kuwajulisha wakazi wote wa Manispaa ya Dodoma na wananchi kwa ujumla kuwa, hivi karibuni kumeibuka kundi la matapeli wanaojitambulisha kwa simu za mkononi kuwa ni watumishi wa Manispaa huku wakitumia vyeo mbalimbali, ikiwemo cheo cha Afisa Mtendaji wa Kata na kuwatapeli wananchi fedha kwa maelekezo kuwa, wanatakiwa kulipia kodi za viwanja na majengo kupitia miamala ya simu.

Matapeli hao wamekuwa wakiwatajia wananchi gharama ya kodi hizo kuwa ni kati ya shilingi 20,000 na 25,000 huku wakiwataka kutuma sehemu ya fedha hizo kwa njia ya simu na kuwaelekeza kuwa, kiasi kilichobaki muhusika akiwasilishe katika Ofisi za Kata husika katika siku watakayokubaliana.

Halmshauri ya Manispaa ya Dodoma inalaani vikali vitendo hivyo na inawataka watu hao kuacha mara moja kwani wanachafua sifa na uhusiano mzuri uliopo baina ya wananchi na watumishi wake hususan watendaji wa Kata, na Halmashauri kwa ujumla.

Halmashauri inafuatilia vitendo hivi kwa karibu na haitosita kuchukua hatua kali za kisheria kwa yeyote atakayebainika kuhusika kwa namna yeyote ile katika vitendo hivyo. Aidha, Mkurugenzi wa Manispaa anawaomba wakazi na wananchi wote kufika na kutoa taarifa ya vitendo vya aina hiyo katika Ofisi za Mtendaji wa Kata husika, Ofisi kuu za Manispaa zilizopo katika Kata ya Viwandani, au katika kituo cha polisi kilichopo karibu.

Ramadhani H. Juma
Ofisa Habari na Uhusiano

22 Juni, 2017